

Video Taping: Eid al Fitr

Adaptor: Khadija

December 3, 2002

Nina furaha kuwaletea ujumbe kwa wote wale wanaosherehekea sikukuu ya Eid al-Fitr, kuhitimisha mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhan.

Ramadhan inaadhimishwa ikiwa ni ufunuo wa neno la Mwenyezi Mungu katika Quran tukufu aliyopelekewa Mtume Mohammed – neno ambalo linasomwa na kughaniwa kwa mtindo maalum na kwa unyenyekevu mkubwa hasa katika kipindi hiki. Mwezi mzima uliopita waislamu walifunga kutokula chakula na kunywa maji wakati wa mchana, ili kulenga mawazo yao kwenye imani na kuelekeza mioyo yao katika kutoa misaada.

Waislamu kote duniani wamenyoosha mikono yao kuwasaidia wale wenye kuhitaji msaada. Meza za vyakula kwa ajili ya watu maskini kuweza kufungua, zilikuwepo mitaani na kwenye miji. Zawadi za chakula, nguo na fedha ziligaiwa ili kuhakikisha kwamba wote wanashirikiana kile mwenyenzi mungu alichowajaalia. Waislamu mara kwa mara huwaalika watu wa dini nyingine kwenye chakula, yaani futari ili kuonyesha imani ya ustahmilivu.

Wakati wa sikukuu ya Eid al-Fitr, waislamu wanasherehekea kumalizika kwa mfungo na kushukuru kwa kupata imani zaidi ambayo imekuja wakati wa mfungo. Tamaduni zinatofautiana baina ya nchi na nchi, kuanzia kwenye mwanga wa kandili huko Misri, mpaka kwenye kuwashwa kwa fataki nchini Pakistan, na hadi Niger ambako watu wazima hukaribishwa chakula cha asili.

Kote duniani, familia, majirani na marafiki hukusanyika pamoja kula pamoja chakula cha kiasili na kupongezana kwa kuweza kuukabili na kuukamilisha mfungo wa Ramadhan.

Sikukuu hii inatukumbusha kwamba Uislamu unaleta matumaini na kuwafaraji mamilioni ya watu nchini kwangu, na mabilioni wengine kote duniani. Ramadhan pia ni wakati wa kukumbuka kwamba Uislamu umezaa ustaarabu wa kujifunza ambao umewanufaisha binadamu.

Hapa Marekani, waislamu wametoa michango mingi katika nyanja ya biashara, sayansi, sheria, afya, elimu na sekta nyingine. Waislamu walioko kwenye jeshi, na kwenye utawala, wanawatumikia wamarekani wenzao kwa heshima, na kutetea ubora wa uhuru wa taifa hili pamoja na haki kote duniani kwa njia ya amani.

Laura anaungana nami kuwatakia kila la kheri na baraka waislamu kote hapa Marekani, na duniani kwa ujumla, kwa ajili ya sikukuu hii yenye furaha tele. Baraka mlizopata wakati wa Ramadhan ziwe pamoja nanyi katika miaka inayofuata.